Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA

LA MTANDAONI | TOLEO LA JUNI 2023

## MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, ALIPOTEMBELEA MRADI WA UJENZI WA HOTELI YA KITALII YA NYOTA TANO INAYOMILIKIWA NA NSSF JIJINI MWANZA



Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**

Simu Bure 0800116773

@NssfTanzania

# HONGERENI SANA, KITU KIZURI

**Na MWANDISHI WETU**

Ni kauli iliyotolewa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati alipotembelea mradi wa ujenzi wa hoteli ya kitalii ya nyota tano inayomilikiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi wa Jamii (NSSF).

Katika ziara hiyo Mhe. Rais Dkt. Samia alitembelea mradi huo uliopo eneo la Capripoint jijini Mwanza tarehe 14 Juni 2023, akiwa amefuatana na viongozi mbalimbali akiwemo Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Mhe. Patrobas Katambi. Alisema Mfuko ukipata mapato mazuri zaidi uangalie kuwekeza kwenye maeneo mengine ikiwemo Dodoma na Dar es Salaam.

“NSSF sasa hii sio fedha yenu ni fedha za wafanyakazi huko nje, mko pale nendeni toeni huduma, ichungeni hiyo fedha ya wafanyakazi ili anapostaafu mtu baada ya utumishi wake akute mzigo wake,” alisema.

Kwa upande wake, Mhe. Patrobas Katambi alisema miradi ya aina hiyo ili ipitishwe ni lazima Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ishauri na Ofisi ya Waziri Mkuu ina jukumu la kusimamia na kwa kuwa lengo la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kuwekeza ni kulinda fedha za Mifuko.

Akitoa maelezo kuhusu mradi huo wa hoteli, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba alisema kukamilika kwa ujenzi wa hoteli hiyo ni vema kukaenda sambamba na kuendeleza uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa sababu watu mbalimbali watakaokuja kwa shughuli za utalii watahitaji kulala katika hoteli hiyo.

“Mheshimiwa Rais Dkt. Samia umbali kutoka hapa Mwanza kwenda Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni Kilomita 140 tofauti na kupitia Arusha ambako ni mbali, kukamilika kwa ujenzi wa uwanja wa ndege Mwanza kutachangia na kuvutia watalii hivyo tunakuomba uwanja ule uendelezwe kwa viwango vya kimataifa,” alisema.



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizungumza mara baada ya kupokea maelezo kuhusu ujenzi wa mradi wa hoteli ya kitalii ya nyota tano inayomilikiwa na NSSF



# MKURUGENZI MKUU NSSF ABAINISHA SABABU ZA KUCHELEWA KUKAMILIKA HOTELI YA KITALII YA NYOTA 5 JIJINI MWANZA

**Na MWANDISHI WETU**

Masha Mshomba, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), amebainisha mbele ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, changamoto kubwa iliyopelekea kuchelewa kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa hoteli ya kitalii ya nyota tano iliyopo jijini Mwanza eneo la Capripoint inayomilikiwa na NSSF ni kutokuwepo kwa muendeshaji hoteli wa kimataifa.

Mshomba amesema hayo mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyetembelea mradi huo tarehe 14 Juni, 2023. Hata hivyo amebainisha kuwa kuanzia mwezi Juni mwaka 2024 hoteli hiyo inatarajiwa kukamilika na kuanza kazi rasmi.

Alisema katika uzoefu walioupata kwa wenzao wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya nchi Jirani ikiwemo Afrika Kusini, Zambia na Zimbabwe ni kwamba huwezi kumalizia hoteli ya nyota tano kabla hujapata muendeshaji wa hoteli.

“Mheshimiwa Rais Dkt. Samia vile hatukupata muendeshaji wa hoteli kipindi kile ndio maana mradi ulishindikana kukamilika,” alisema Mshomba.



**Inaendelea ...**

Alisema ilipofika mwaka 2017/18, Mfuko ulitangaza zabuni ya muendesha hoteli hata hivyo hakupatikana kutokana na mazingira ya kipindi hicho na mwaka 2019 mwezi Septemba walienda nchini Zambia na Afrika Kusini ili kupata uzoefu jinsi Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya nchi hizo inavyopata waendeshaji wa hoteli ambapo NSSF ilipata kampuni ya *Hilton Hotels Worldwide, Radissons Hotels na Legacy Hotel.*

Mshomba alisema ilipofika mwezi Machi 2021, shughuli za ujenzi ziliendelea na walianza kumtafuta msanifu wa kuandaa michoro na mahitaji muhimu kwa ajili ya kumalizia kazi za ndani kwa viwango vya kimataifa *(Interior Designer Architect) M/s SOURCE IBA* toka Afrika Kusini.

Alisema mwezi Septemba 2022 walitangaza zabuni ya kumpata muendeshaji hoteli wa kimataifa, na kwamba kipindi hicho zile kazi ambazo zinahitajiwa kuendelea kabla ya kuwa na muendeshaji hoteli zilikuwa zinaendelea kama vile ujenzi wa vyoo na madirisha.

Mshomba alisema mpaka sasa baada ya kutangaza zabuni wamewapata waendesha hoteli watatu ambao waliomba zabuni ikiwemo kampuni ya *Hilton Hotels Worldwide, Radissons Hotels na Legacy Hotel*, ambapo mwishoni mwa mwezi huu wanatarajia kupata mshindi.

Alisema baada ya kupatikana kwa muendeshaji hoteli, wanatarajia hadi kufika mwezi Juni 2014 ujenzi wa hoteli hiyo uwe umekamilika na kwamba itachangia sana shughuli za kitalii jijini Mwanza.

# MUENDESHAJI HOTELI WA KIMATAIFA NI KIGEZO CHA MSINGI KATIKA KUKAMILISHA MRADI WA HOTELI YA KITALII YA NYOTA TANO

**Na MWANDISHI WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amesema katika ujenzi wa hoteli za nyota tano muendeshaji wa hoteli mwenye hadhi ya kimataifa ni kigezo cha msingi katika kukamilisha mradi wa aina hiyo.

Mshomba alieleza hayo tarehe 14 Juni, 2023 mbele ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyetembelea mradi wa hoteli ya nyota tano inayomilikiwa na NSSF iliyopo jijini Mwanza.

"Katika ujenzi wa hoteli za nyota tano kwa uzoefu ambao tuliupata kutoka kwa wenzetu wa Mifuko kama sisi wa nchi jirani, kwa mfano Afrika Kusini, Zambia na Zimbabwe ni kwamba huwezi kumalizia hoteli kama hii kabla hujampata yule muendesha hoteli," alisema Mshomba.

Alisema kwa vile jambo hilo halikuwezekana ndio maana mradi wa hoteli hiyo ulisimama na kwamba mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi huu wa Juni 2023 wanatarajia kumpata muendeshaji wa hoteli na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2024.

Kwa mujibu wa Mshomba, mwaka 2019 walienda kujifunza nchini Zambia na Afrika Kusini ili kupata uzoefu jinsi wanavyopata waendeshaji hoteli ya kitalii ya nyota tano.

"Kule tuliweza kuwapata kampuni kama *Hilton Hotels Worldwide* ambao walikuwa wanaendesha hoteli kule, lakini pia *Radissons Hotels na Legacy Hotel*, ambapo tuliongea nao lakini kwa bahati mbaya mwishoni mwa mwaka 2019 ukazuka ugonjwa wa Corona (COVID 19) uliosababisha mambo mengi kusimama.

Hata hivyo, Mshomba alisema ilipofika mwezi Machi 2021, shughuli za ujenzi ziliendelea na walianza kumtafuta msanifu wa kuandaa michoro na mahitaji muhimu kwa ajili ya kumalizia kazi za ndani kwa viwango vya kimataifa *(Interior Designer Architect) M/s SOURCE IBA* toka Afrika Kusini.

Alisema mwezi Septemba 2022 walitangaza zabuni ya kumpata muendesha hoteli wa kimataifa, na kwamba kipindi hicho zile kazi ambazo zinahitajiwa kuendelea kabla ya kuwa na muendesha hoteli zilikuwa zinaendelea kama vile ujenzi wa vyoo na madirisha.

Mshomba alisema baada ya kutangaza zabuni wamewapata waendesha hoteli watatu ambao waliomba zabuni ikiwemo kampuni ya *Hilton Hotels Worldwide, Radissons Hotels na Legacy Hotel,* ambapo mwishoni mwa mwezi huu Juni 2023 wanatarajia kupata mshindi.

Akizungumza katika mradi huo, Mhe Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliipongeza NSSF kwa mradi wa hoteli hiyo kuwa ni kitu kizuri ambapo itakapokamilika itachochea sekta ya utalii na kuongeza tija kwenye Mfuko.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba akitoa maelezo kwa Mhe. Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhusu ujenzi wa mradi wa hoteli ya kitalii ya nyota tano inayomilikiwa na NSSF iliyopo jijini Mwanza.



Meneja Usimamzi wa Miradi NSSF, Mhandisi Helmes Pantaleo akitoa maelezo kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania namna mradi wa hoteli ya kitalii ya nyota tano utakavyokuwa.

# RAIS DKT. SAMIA: VITEGA UCHUMI KAMA HIVI VITAONGEZA TIJA KWA NSSF

**Na MWANDISHI WETU**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema miradi ya vitega uchumi inayofanywa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) itaongeza tija kwenye Mfuko.

Amesema hayo tarehe 14 Juni, 2023 wakati alipotembelea mradi wa ujenzi wa hoteli ya kitalii ya nyota tano inayomilikiwa na NSSF iliyopo katika eneo la Capripoint jijini Mwanza.

Mhe. Rais Dkt. Samia ameipongeza NSSF kwa mradi wa hoteli hiyo kuwa ni kitu kizuri ambapo itakapokamilika itachochea sekta ya utalii na kuongeza tija kwenye Mfuko. "Hongereni sana NSSF kwa kweli mradi huu ni kitu kizuri," alisema Mhe. Rais Dkt. Samia.

Alisema anaamini kuwa wataalamu wameshapiga mahesabu kuwa mradi huo utakuwa na tija kwa NSSF na Taifa kwa ujumla, na kwamba Mfuko ukipata mapato mengi zaidi uangalie na maeneo mengine ya kuwekeza kama vile Dodoma.

Mhe. Rais Dkt. Samia aliwaagiza wafanyakazi wa NSSF kuendelea kutoa huduma bora na kuchunga fedha za wanachama ili wanapostaafu waweze kulipwa mafao yao mara moja.



**Inaendelea ...**

Naye, Mhe. Patrobas Katambi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, alisema Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inawekeza kwa lengo la kulinda thamani ya michango ya wanachama na kuahidi kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaendelea kushirikiana na Mfuko katika kuangalia maeneo mengine ya uwekezaji.

Akitoa maelezo ya mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Msomba alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2024 na kwamba kukamilika kwa hoteli hiyo kutachangia shughuli za kiuchumi katika jiji la Mwanza ukizingatia kuwa jiji hilo lina shughuli nyingi za kiuchumi ikiwemo uvuvi na madini.

Alisema ujenzi wa hoteli hiyo ni vema ukaenda sambamba na uendelezaji wa uwanja wa ndege wa Mwanza kwa sababu watu watakao kuja kwa ajili ya utalii watahitaji kulala katika hoteli hiyo hasa ukizingatia kuwa umbali wa kutoka Mwanza hadi Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni takribani Kilomita 140.

Akitoa maelezo ya hoteli hiyo, Mhandisi Helmes Pantaleo ambaye ni Meneja Usimamizi wa Miradi wa NSSF, alisema hoteli hiyo ina jumla ya ghorofa 16, vyumba 168 vya kulala vya aina mbalimbali ikijumuisha sehemu ya kupumzikia Rais (Presidential Suite), migahawa, sehemu za vinywaji na michezo (sports bar).

Pia, kuna ukumbi mkubwa wa mikutano wa kuchukua watu 500, kumbi ndogondogo za mikutano, bwawa la kuogelea, sehemu za kufanyia mazoezi, ofisi, maduka, sehemu ya maegesho ya magari na juu kabisa ya jengo hili kuna sehemu ya kutua chopa (helkopta).

# MATUKIO KATIKA PICHA ZIARA YA MHE. RAIS DKT. SAMIA MRADI WA UJENZI WA HOTELI YA KITALII YA NYOTA 5 MWANZA













Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF